

# CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

S.L.P. 35091 ♦ DAR ES SALAAM ♦ TANZANIA



## TAARIFA KWA UMMA

### MAHAFALI YA 48 YA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani, kinapenda kuwataarifu wadau wa Chuo na umma kwa ujumla kuwa kitafanya **Mahafali ya Arobaini na Nane (48)** mwezi Novemba 2018 katika Ukumbi wa Mikutano wa Mlimani City. Mahafali haya yamegawanyika katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni la kutunuku Shahada za Uzamivu, Umahiri na Stashahada za Uzamili, pamoja na wa Shahada za Awali kwa wahitimu wa Ndaki ya Teknolojia za Habari na Mawasiliano; Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia; Ndaki ya Sayansi za Kilimo na Teknolojia za Uvuvi; na Ndaki ya Sayansi Asilia na Tumizi. Kundi hili litafanya mahafali yake **Jumane Tarehe 13 Novemba 2018 kuanzia Saa Tatu Asubuhi**. Kundi la pili litakalofanya mahafali **Jumamosi tarehe 17 Novemba 2018 kuanzia Saa Tatu Asubuhi** litawahusu wahitimu wa shahada za awali zilizobakia, yaani kutoka Ndaki ya Sayansi za Jamii, Ndaki ya Insia, Shule Kuu ya Elimu, Shule Kuu ya Biashara, Shule Kuu ya Sheria, Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma, Taasisi ya Taaluma za Maendeleo, na Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Mwaka huu kutakuwa na jumla ya wahitimu **4,742**. Kati yao **74** watatunukiwa Shahada ya Uzamivu, **435** Shahada za Umahiri, **15** Stashahada ya Uzamili na wahitimu **4,137** watatunukiwa Shahada za Awali na **81** watatunukiwa Stashahada na Astashahada.

#### Mchanganuo wa wahitimu kwa tuzo husika ni kama ifuatavyo:

| NA. | TUZO  | WANAUME      | WANAWAKE     | JUMLA        | % KE         |
|-----|---|--------------|--------------|--------------|--------------|
| 1   | Shahada ya Uzamivu ( <i>PhD</i> )                     | 16           | 58           | 74           | 21.62        |
| 2   | Shahada ya Umahiri ( <i>Masters Degree</i> )          | 155          | 280          | 435          | 35.63        |
| 3   | Stashahada za Uzamili ( <i>Postgraduate Diploma</i> ) | 7            | 8            | 15           | 46.67        |
| 4   | Shahada za Awali ( <i>Bachelors</i> )                 | 1,542        | 2,595        | 4,137        | 37.27        |
| 5   | Stashahada na Astashahada (Non Degrees)               | 21           | 60           | 81           | 25.93        |
|     | <b>Jumla Kuu</b>                                      | <b>1,741</b> | <b>3,001</b> | <b>4,742</b> | <b>36.71</b> |

Kabla ya kuanza rasmi kwa shughuli za kundi la kwanza ya mahafali ya 48 hapo tarehe 13 Novemba 2018, Amidi Mkuu wa Sherehe (**Dean of Ceremonies**) za Chuo atasimikwa rasmi na kukabidhiwa vitendea kazi kutoka kwa aliyekuwa Amidi Mkuu wa Sherehe Prof. Bonaventure Rutinwa ambaye sasa ni Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Taaluma). Uongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam unawakaribisha wadau wote wa elimu ya juu kuhudhuria na kushiriki katika mahafali hayo.

Imetolewa na

Prof. William A. L. Anangisye

**Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**